



Hudumu kwa  
muda mrefu,  
muda mrefu zaidi!

National  
SPECIAL



# UHURU



Na. 3,231

JUMAMOSI, JANUARI 25, 1975

Bei Senti 36

Salim awaambia wanachuo:

## Ukombozi ni jukumu la wananchi

Na Joe Nakajumo

UHURU katika makoloni utapatikana tu kutokana na juhud za wananchi wenyewe na wala hautaletwa na Umoja wa Mataifa ambao msimamo wake katika suala hilo ni kuhimiza tu shughuli za ukombozi, Mjumbe wa kudumu wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, Ndugu Salim A. Salim alisema mjini Dar es Salaam juzi usiku.



NDUGU SALIM

Ndugu Salim amriye alikuwa akiwahutubia wanafunzi na walimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juzi jioni juu ya wajibu uneotekelezwa na Umoja wa Mataifa katika kuondoa ukoloni. Alisema hatua siku moja heitatakeea kwa Umoja huo kwenda katika koloni fulani na kutoa uhuru kwa mabavu. "Kazi ya kutwaa Uhuru itafanywa na wazalendo wenyewe na Umoja wa Mataifa utakuwa ukiwahimiza na kuwaunga mkonono tu wananchi hadi katika harakati za kujikomboa", alisisitiza Ndugu Salim.

Mjumbe huyo wa kudumu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya mataifa 24 ya Umoja huo inayoshughulika na kuondoa ukoloni, alisema kazi ya kamati hiyo ni kusisitiza utekelezaji wa lengo lake la kuondoa ukoloni, na kuyashawishi mataifa mengine kungia katika mkindo wa ukondoa ukoloni.

Ndugu Salim alieleza pia kwamba katika makoloni mengine madogo mengi yao yakiwa ni visiwa vidogo vyenye watu wachache sana, wakoloni wanotaawala makoloni hayo wanakuwa vichwangu kwa kudai kwamba watu wachache namna hiyo hawawezi kupewa haki ya kujitawala. Kutokana na hali hiyo, Ndugu Salim alionya kwamba haki ya kujitawala ni kwa wote, liwe taifa dogo lenye watu wachache au lenye mamiloni ya watu.

Mjumbe alieleza ugumu mwingine wa kuondoa ukoloni unaosababishwa na mataifa makubwa kwa kuvunja vikwazo vya Umoja wa mataifa dhidi ya tawala dhaili mu na akatoa mfano wa Marekani ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa iliyokubali kuuveeka vikwazo vya biashara utawala haramu wa Rhodesia, lakini inashiriki katika kuvivunja vikwazo hiyo.

Alisema nchi za Afrika, Latin Amerika na Asia, zina imani na kuheshimi maazimio ya Umoja wa Mataifa kuliko yanavyofanya mataifa makubwa. Aliongeza kwamba baadhi ya mataifa yaliyo na wajumbe wa kudumu katika Baraza la Usalama yana hisa huko Namibia.

Ndugu Salim alisema Umoja wa Mataifa unapata ushirikiano mkubwa kutoka New Zealand na Australia katika juhud za kuondoa ukoloni katika visiwa vinavyomilikiwa na nchi hizo katika bahari ya Pacific. Aliongeza kwamba Ufaransa ambayo pia inamiliki visiwa vyake huko pamoja na koloni la Ufaransa la Somalia, haina ushirikiano hata chemba

kwani inayanesabu makoloni hayo kama ni majimbo yake ya ngamoto.

Aieleza kuwa mwaka huu una-fanana kwa kuwa na mafanikio na mwaka 1960 wakati ambapo nchi 15 za Kiafrika ziliingia kwenye uanachama wa Umoja wa Mataifa na mwaka huu kuna mategemeo ya Msumbiji, Angola, Muungano wa Guinea-Bissau na visiwa vya Cape Verde, Sao Tome Seychelles na Comoro, kuingia kwenye Umoja huo baada ya kupata uhuru.